

## Uainishaji wa Mafumbo ya Wosia wa Babu kwa Wavulana Miongoni mwa Wabukusu wa Kenya.

John Swala Barasa Wangila<sup>1</sup>; Wandera-Simwa, Sheila<sup>2</sup>; Onyango J. Ogola<sup>3</sup>

Laikipia University, Kenya

Main author email: [johnswala@gmail.com](mailto:johnswala@gmail.com)

Utafiti huu ulidhamiria kuainisha mafumbo ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa Wabukusu wa Kenya. Madhumuni ya makala hii yalikuwa kuainisha mafumbo yanayotumiwa katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa Wabukusu wa Kenya. Uandishi wa makala hii ulitumia nadharia ya umitindo iliyoasisiwa na Leech (1965). Nadharia hii huhimiza umuhimu wa mitindo tofauti ya lugha katika fasihi. Data za makala hii zilikusanywa kutoka kata mbili za wilaya ya Kimilili. Muundo wa kimatelezo ulitumika kuwasilisha na kuchanganua data. Mbinu za mahojiano na uchunzaji wa kushiriki zilitumika kukusanya data. Sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuwachagua wazee wanne wa kati ya miaka sitini na sabini na wavulana wanne wa kati ya miaka kumi na nane hadi ishirini na mbili kutoka kata zizo hizo ili kushiriki katika utafiti. Utafiti ulibainisha kuwa babu hutumia mafumbo ya vitendawili, mafumbo ya jazanda, mafumbo ya majina, mafumbo ya maonyo, mafumbo ya miko na chemshabongo katika wosia wao kwa wavulana. Makala hii ina manufaa kwa wanafunzi na wataalamu wa fasihi simulizi, shuleni na vyuoni, kwa kuwafahamisha kuhusu aina ya mafumbo yanayotumika katika jamii ya Wabukusu na jamii zingine. Makala hii inapendekeza kuwa vyombo vya habari viwe vikipeperusha hotuba za wosia unaotumia mafumbo kwa wananchi ili kuwafikia watu wengi. Kwa kufanya hivi, wavulana wengi watapata ujumbe uliomo kwenye mafumbo haya na wataimarika kitabia.

**Maneno muhimu:** Mafumbo, wosia, babu, wavulana.

\*\*\*

### How to cite this article in APA (6<sup>th</sup> Edition)

Wangila, J. S. B., Wandera-Simwa, S.P.; Ogola, J. O. (2021). Uainishaji wa Mafumbo ya Wosia wa Babu kwa Wavulana Miongoni mwa Wabukusu wa Kenya. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 2(1), 223-230. DOI: <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.206>

\*\*\*

## UTANGULIZI

Waluhya wanaishi mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Waluhya ni mwavuli wa jamii zingine ndogondogo kama vile Maragoli, Batachoni, Watiriki, Wanyala, Baesukha, Wakabarasi, Waitakho na Wabukusu (Simiyu, 2015). Wabukusu wana fasihi yao inayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia sherehe za baada ya tohara. Kulingana na Wasike (2017), Wabukusu hupitisha utamaduni wao kutumia mafumbo. Utamaduni huu hupitishwa kwenye wosia unaotolewa na babu kwa wavulana baada ya sherehe ya tohara kuwaandaa wavulana kwa maisha ya utu uzima. Mafumbo ni kipera cha utanzu wa semi wa fasihi simulizi. Makala hii iliainisha mafumbo yanayotumika katika wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa Wabukusu wa Kenya.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Mafumbo ni kipera cha utanzu wa semi katika fasihi simulizi. Mafumbo yamefafanuliwa kwa njia mbalimbali na wataalam tofauti tofauti wa fasihi simulizi. Kulingana na kamusi ya TUKI (2014), fumbo ni jambo lisilojulikana au ni maneno yasiyojulisha maana yake waziwazi. Fumbo ni maneno yenye maana isiyojulikani kwa wahusika. Kulingana na Ayiera (2017), mafumbo huelezea kauli zilizoficha maana. Mafumbo huwa ni jambo lililofichwa na huhitaji kujibiwa au kutoa maelezo ya kulifafanua. Makala hii ilichukulia mafumbo kuwa ni majina, maneno au vifungu vya maneno vinavyotumia vitu vinavyopatikana katika mazingira ya jamii husika kwa kutumia lugha ya kisania ili huficha maana ya kitu.

## Nadharia ya Umitindo

Chemutai (2016) anadai kuwa nadharia ya umitindo iliasisiwa na Leech (1965). Nadharia ya umitindo ina misingi yake nchini Urusi. Nadharia hii ilibuniwa kueleza upekee wa lugha ya kifasihi hasa ushairi kwa sababu mashairi ndiyo maandishi yaliyokuwepo wakati huo. Wananadharia hii hudai kuwa mtindo hutegemea fanani

kwani ni yeye huchagua lugha anayotaka kutumia (Gathenya, 2018). Mtindo ndio humtofautisha mzungumzaji mmoja na mwingine kwa sababu ya matumizi ya mitindo tofautitofauti. Wazungumzaji hutumia lugha tofauti kwani kila mmoja huwa na uchaguzi wake wa msamiati, jazanda, tamathali za usemi, miundo ya sentensi na wasifu wa kisarufi. Kila babu katika jamii ya Wabukusu huteua mtindo wake tofauti wa kutumia lugha. Nadharia ya umitindo ina kipengele kuhusu kiwango cha msamiati ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, tashbihi, istiari na mafumbo. Kipengele hiki kilitumiwa kuainisha mafumbo kama mbinu inayotumiwa katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana katika jamii ya Wabukusu.

## MBINU ZA UTAFIGI

Makala hii ilitumia muundo wa kimaielezo kwa sababu data zilikuwa za kithamano. Kimaeneo, utafiti ulifanywa wilayani Kimilili kwa sababu kuna Wabukusu wengi wanaofoata mila za Kibukusu kama vile kuwapa wavulana wosia baada ya tohara ili kuwatayarisha kwa maisha ya utu uzima. Utafiti uliwalenga babu wa kati ya miaka sitini na sabini na wavulana wenye umri wa miaka kati ya kumi na nane hadi ishirini na mbili. Sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuchagua sampuli ya utafiti. Mbinu ya mahojiano na uchunzaji wa kushiriki zilitumiwa kukusanya data huku mbinu ya kimaielezo ikitumiwa katika uchanganuzi na uwasilishaji data. Makala hii ilieleza ujumbe ambao ulipatikana kutumia uchunzaji wa kushiriki na mahojiano. Nadharia ya umitindo ilitumiwa katika uchanganuzi wa data.

## MATOKEO

### Uainishaji wa Mafumbo

Uainishaji ulifanywa kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya umitindo unaosema kuwa katika kiwango cha msamiati mtafiti wa fasihi hujishughulisha na uteuzi wa

mbinu kama vile jazanda, tashbihi, istiari na mafumbo ambazo hutumiwa katika uwasilishaji wa kazi za fasihi. Uainishaji huu ulifanywa kwa kutumia sifa zinazotofautisha aina moja ya mafumbo na nyingine. Wasike (2017) anadai kuwa Wabukusu hupasha mila zao kwa vizazi vijavyo kwa kutumia mafumbo. Utafiti huu uliainisha mafumbo yafuatayo katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana katika jamii ya Wabukusu.

#### **Mafumbo ya Majina**

Kwa mujibu wa wahojiwa, wazazi katika jamii ya Wabukusu huwaita watoto majina yenye maana fiche. Majina haya hutumiwa katika wosia wa babu kwa wavulana kwa nia ya kutoa mafunzo kwa wavulana hao. Waswahili huwapa watoto majina kulingana na mazingira ambamo watoto hao wamezaliwa (Sauda, 1994). Katika fasihi andishi, mwandishi huwapa wahusika wake majina ya kimafumbo ili kuficha ujumbe ulio kwenye matini (Ayiera, 2017). Mberwa, (2015) anadai kuwa majina ya mimea ya kimatibabu hutajwa kimafumbo. Majina ya mafumbo hayahitaji majibu ya haraka lakini huwahitaji wavulana kufikiria maana ya majina husika. Jamii ya Wabukusu hutumia majina yafuatayo katika harakati za kuficha ujumbe fulani;

#### **Kundu (Jitu)**

Hili ni jina wanaopewa watoto wavulana waliofiwa na wenzao pindi wanapozaliwa. Kuna uwezekano wa watoto kufa baada ya kuzaliwa kwa kufuatana. Kwa mfano, watoto watatu wakizaliwa na kufa mmoja baada ya mwingine, yule atakayezaliwa wa nne atapewa jina *Kundu* ili kukinga kifo.

#### **Wafubwa**

Hili ni jina la kimafumbo linalooleanwa kwa mtoto aliyebaki pekee yake baada ya wenzake kufariki. Jina hili huwa jina la pili la mtoto. Kwa mfano familia ikiwa na watoto wanne ambao wamepewa majina kisha watatu

wao wafariki kwa hali yoyote ile, yule atakayebaki hupewa jina *Wafubwa* kumlinda dhidi ya kifo.

#### **Walekhwa (Aliyebaki)**

Hili linalooleanwa kwa mtoto mvulana ambaye mama yake alifariki akiwa bado mchanga. Katika wosia, babu hutumia jina hili kuonyesha jinsi jamii ya Wabukusu hukabiliana na mikasa ya watoto kuachwa na mama yao wakiwa wachanga. Jina hili hutumiwa kuonyesha umoja wa Wabukusu wakati wa shida.

#### **Bulala (Umoja)**

Hili ni jina la kimafumbo ambalo watoto wavulana wanaozaliwa wakati kuna mikutano hupewa. Jina hili huficha ujumbe unaopatikana katika mikutano hiyo kwani huweza kuwa mikutano ya kusuluhisha migogoro katika maisha ya wazazi wake.

#### **Kumusola**

Ni jina la mti. Jina hili linamaanisha mti huu huandoa kisirani na matata katika mji. Hali hii ni sawa na utafiti wa Mberwa, (2015) uliodhihirisha kuwa waganga hutumia majina ya kimafumbo kutaja miti inayotumiwa katika matibabu ili kuficha siri za uganga wao.

#### **Mafumbo ya Maonyo**

Mafumbo ya maonyo huwahimiza wavulana kujitenga na vitendo vibaya vinavyoweza kuathiri maisha yao. Kulingana na Sauda (1994), mafumbo ya maonyo hutumiwa kuwakashifu viongozi wanaotenda mambo mabaya kwa wananchi. Wabukusu hawatumii lugha wazi katika maonyo kwa sababu wazee katika wosia wao hulenga wavulana mahususi, wale wa jamii yao pekee. Mafumbo ya maonyo hayahitaji majibu papo hapo bali wavulana hujiwekea majibu hayo akilini ili yawasaidie baadaye. Maonyo huwa fupi sana ili wavulana waweze kuyakumbuka haraka. Tamathali za usemi hutumiwa kuficha ujumbe ulio kwenye fumbo.

*Obe omundu omurekerefu okhaba nga mbarakala tawe.*  
*Obe omwana omurekeru, oayaaya sakhusia kumusanga tawe.*

Tafsiri

*Uwe mtu anayesikia maneno usiwe na kiburi kama mbakara.*

*Uwe mwana msikivu, anayerukia maneno hashiki mkuki.*

Ni maneno yanayowaonya wavulana wasiwe wenye pupa. Wavulana wanaelezwa wawe makini kwa yale wanayoambiwa na watu wengine hasa wanaowazidi kwa umri. Fumbo hili limetumia tashbihi kama mbinu ya lugha. Kiburi kinalinganishwa na tabia ya *mbarakala* ambaye Wabukusu wanaamini ana kiburi sana. Neno mkuki limetumiwa kijazanda kuashiria mtu mwenye pupa anaweza kutumia vitu hatari kufanya maovu katika jamii.

*Okhekomba mao tawe.*

Tafsiri

*Usimtamani mama yako.*

Hili ni fumbo linalowaonya wavulana dhidi ya kuwatamani wanawake wenye umri mkubwa kuwaliko, hasa wale walio na umri sawa na ule wa akina mama yao. Inaaminika kuwa mwanamke yeyote aliye na umri sawa na wa mamako ni mama.

*Omwana omulianga omubi, okhaboa bulianga khumunwa tawe.*

Tafsiri

*Mtoto mlafi ni mbaya, usifunge ulafi mdomoni.*

Hili ni fumbo la kuwaonya wavulana dhidi ya ulafi kwa sababu maovu yote duniani husababishwa na ulafi. Ulafi husababisha wizi na mauaji miongoni mwa wavulana.

*Omwana umulai okhaboa chisilingi khwineke tawe.*

Tafsiri

*Mtoto mzuri usiweke pesa zako kwenye uume wako.*

Fumbo hili linawaonya wavulana wasitumie mali yao kuwafurahisha wanawake ili wapendwe. Fumbo lililo

kwenye maneno haya hutumiwa kuwafunza wavulana kuhusu mbinu nzuri za kutumia mali walizochuma ili zivasaidie katika maisha yao. Fumbo hili linaonya wavulana dhidi ya makahaba na anasa.

*Olabira khuluchi okhaswena khukhabale tawe.*

Tafsiri

*Ukivuka mto usikanyage kijiwe.*

Mito huwa na vijawe ambavyo mtu anaweza kukanyaga na kumsaidia kuvuka mto huo. Hii ni hatari kwa sababu huenda jiwe hilo liwe ndogo na lililoelea juu ya maji na unapolikanyaga unaweza ukazama majini. Hili ni fumbo ambalo huwaonya wavulana dhidi ya kutotazama jambo kwa makini kabla ya kuanza kulitenda.

*Nocha abundu okhalola efula tawe, lola kamafumbi.*

Tafsiri

*Ukiwa safarini usiangalie mvua, angalia mawingu.*

Fumbo hili linamaanisha kuwa wavulana katika jamii ya Wabukusu wanastahili kuangalia dalili ya jambo fulani kama jambo lenyewe halijatendeka. Wavulana wanashauriwa wasingoje jambo mbaya litendeke ndipo waanze kutafuta suluhisho bali wakiona dalili ya shida, waanze kutafuta suluhisho kabla shida kuwafikia.

*Okhaila nafokoyo tawe.*

Tafsiri

*Usioe mke mvivu.*

Wavulana wanaonywa dhidi ya kuoja wake wavivu kwa sababu hiki ndicho chanzo cha umaskini na shida zingine katika jamii. Wavulana huonywa wasitangamane na watu ambao hawapendi kazi kwa sababu ni kupitia kazini ndipo mtu akapata mahitaji yake ya kila siku.

*Okhakenda nende wepalapacha tawe.*

Tafsiri

*Usitembee na mtu mwenye anapenda kuongea sana au mtu mwenye anapenda kuzungumza sana.*

Fumbo hili huwaonya wavulana dhidi ya kutembea na watu ambao huongea sana kwa sababu huenda wakatoa siri zao kwa watu wa nje.

*Noli nende embelekeu olekhe, embelekeu seli endai tawe.*

Tafsiri

*Wacha tabia mbovu, tabia mbovu si nzuri.*

Fumbo hili huonya wavulana dhidi ya tabia mbovu katika jamii kwa sababu zina madhara mabaya kwa jamii nzima. Huweza kusababisha laana.

*Okhaba ling'ang'ule tawe.*

Tafsiri

*Usiwe mkware.*

Fumbo hili linawaonya wavulana dhidi ya kufanya mapenzi kiholela. Wavulana wanaonywa hivi kwa sababu ya madhara ambayo yanaweza kuwapata ikiwa hawawezi kuzingatia maadili mema katika maisha yao ya kimapenzi.

### Mafumbo ya Miko

Jamii ya Wakamba ina maneno yasiyosemwa mbele ya watu wenye umri mdogo (Nguta, 2013). Jambo hili ni sawa hata katika jamii ya Waswahili ambapo maneno yasiyoruhusiwa kusemwa waziwazi huwasilishwa katika mafumbo (Beck, 2013). Katika jamii ya Wabukusu, wazee hawaruhusiwi kutamka maneno fulani mbele ya wavulana au watoto bali hutajwa kwa kutumia lugha fiche.

*Nonywele kamalwa ko omwana muchuli sawima khusili tawe.*

Tafsiri

*Ukinywa pombe ya mtoto kesho yake usipande kwenye kilima.*

Hili ni fumbo linalowaonya wavulana kuwa baada ya kunywa pombe kwenye sherehe ya kumtahirisha mtoto wa mwenziwe asijiingize katika tendo la ngono. Kwa hivyo *khunina khusili* katika lugha ya kawaida humaanisha

kupanda kilima lakini kimafumbo usemi huu humaanisha tendo la ngono. Kutaja ngono mbele ya wavulana au watoto katika jamii ya Wabukusu ni mwiko kwa wazee.

### Mafumbo ya Jazanda

Jazanda hutumiwa kuficha ujumbe katika mawasiliano, kukuza uwezo wa wavulana wa kufikiria ili kupata kile kinachosemwa. Mwandishi wa riwaya za *Walenisi* na *Mafuta* alitumia jazanda ili kufumba ujumbe ulio kwenye riwaya kwa nia ya kuwazindua wasomaji (Ayiera, 2017). Simiyu (2015) aligundua kuwa wazee katika jamii ya Wabukusu hutumia jazanda katika mazungumzo yao ili wasichukize watu kwa kutaja majina au hali mbalimbali katika jamii. Mafumbo ya jazanda yanayopatikana katika jamii ya Wabukusu ni yafuatayo;

*Kumuliango kumwikule kukwoo, kumwikale kwabene.*

Tafsiri

*Mlango ulio wazi ni wako na uliofungwa ni wa mwenyewe.*

Mlango umetumiwa kumwashiria mwanamke au msichana. Mlango kufungwa ni hali ya mwanamke kuwa ameolewa. Kwa hivyo wavulana huonywa dhidi ya kuwatongoza wanawake ambao wameolewa. Mlango kuwa wazi ni hali ya mwanamke kuwa hajaolewa. Kwa hivyo, ana uhuru wa kutembea na yeyote, kuenda kokote kwa sababu hajafungwa na mtu au hali yoyote.

### Mafumbo ya Vitendawili

Wabukusu hutumia vitendawili kama mafumbo ili kuficha ujumbe unaosemwa. Kulingana na Kipacha (2014), vitendawili ni kijitanzu cha mafumbo ambacho ni semi fupi iliyoficha wazo fulani ambalo ndilo jibu la fumbo hilo. Vitendawili vya Uswahilini ni sawa na vile vya jamii za Kibantu kwa sababu vyote huwasilishwa kwa njia ya maswali yanayohitaji majibu (Ngonyani, 2015). Majibu au maana ya vitendawili hupatikana baada ya kuyatazama mazingira ya jamii kwa makini. Mifano ya vitendawili ni;



Namnaii: *Nalomaloma babandu besindukha.*

Lijibu: *Eradi*

Tafsiri

*Akizungumza watu hushtuka.*

Jibu: *Radi*

Kitendawili hiki kinaashiria kuwa kuna kitu kinapozungumza binadamu hushtuka. Kitendawili hiki kimetumia mbinu ya tashhisi kuipa radi sifa ya kuzungumza ambako kunawezekana tu kwa binadamu. Kwa hivyo Kwa hivyo mteguaji anapaswa kufikiria kile kitu kinachotoa sauti ya kushtua watu.

*Menyile nende umundu mala arera bhutinyu kila siku.*

Jibu: *Embalikha*

Tafsiri

*Naishi na mtu na huleta shida kila siku.*

Jibu: *Ukewenza*

Kitendawili hiki kinaashiria kuwa kuna kitu ambacho mteguaji anaishi nacho na humletea shida kila mara. Jibu ni ukewenza kwa sababu ni hali ambayo mwanamke anaweza kuishi nayo na isimpe furaha wakati wowote. Kitendawili hiki huambiwa wavulana waepuke kuoa wake wengi kwa sababu hawatakuwa na amani katika maisha yao.

Namnaii: *Bhuli omundu ali nende khamocha lukongo.*

Lichibu: *Bikele*

Tafsiri

*Kitendawili: Kila mtu ana gari.*

Jibu: *miguu*

Hiki ni kitendawili ambacho humwitaji mvulana kufikiria kitu ambacho kila mtu anacho na humsaidia katika usafiri. Gari katika kitendawili hiki limetumiwa kimaumbo kumaanisha miguu.

Namnaii: *Sai akoloba mala wenya khuja lukendo lwa akarikari we edesati. Bakhuwele erusa eya khuchaguwa bindu bitaru khubino; likabuti, kumubano, kimiwani,*

*etochi, sikioo nende kamechi. Olachaguwa sina na khubela sina?*

Jibu: *Ndachaguwa etochi, khubela lukendo lwe musilo nilwo nende sisilima. Kumubano, onyala warumikhila nga bulwani musilo.*

*Kamechi, khubela lukendo lwe mudesati luluya lukali.*

Tafsiri

fumbo: *Ni jioni na unataka kuanza safari katikati mwa jangwa. Umpewa ruhusa ya kuchagua vitu vitatu kati ya hivi; kabuti, kisu, miwani, kurunzi, kioo na maji. Utachagua nini na kwa nini?*

Jibu: *Nitachagua, kurunzi kwa sababu safari ni ya usiku na kutakuwa na giza. Kisu kwa sababu kinaweza kutumiwa kama silaha wakati wa usiku. Maji kwa sababu jagwani huwa na jingi na huenda nikahisi kiu.*

Fumbo hili linaashiria vitu vinavyohitajika safarini. Tunagundua kuwa siyo kila kitu hutumiwa katika safari zote. Fumbo hili ni funzo pia kwa wavulana ili wajue kujipanga mapema kwa maisha ya baadaye. Huwasaidia kujua ni nini kitahitajika wakati fulani na kipi hakitahitajika.

Namnaii: *Omundu, omukhai wewe, mai wewe nende mai omukhwe Belukha liye musirekere mwabwe. Babandu berana sana. Ngabola karibu nende luluchi, banyola liliaro liliambusha bandu bataru bong'ene. Balekha nanu afwile muliye?*

Jibu: *Mai omukhwe. Sakekhala alala nende omusecha owa omwana tawe.*

Tafsiri

Namnaii: *Mtu, mkewe, mama yake na mama mkwe walitoroka vita vilivyokuwa kijijini mwao. Walipofika karibu na mto walipata mtumbi wa kuvusha watu watatu pekee. Nani angeachwa auawe katika vita?*

Jibu: *Ni mama mkwe kwa sababu hawezi keti pamoja na mume wa mtoto wake.*

Hili ni fumbo ambalo hufumba mila na utamaduni wa jamii ya Wabukusu. Katika jamii hii mvulana haruhusiwi kukaa

pamoja na mama mkwe wake. Kwa hivyo fumbo hili huwaonya wavulana kuzuia njia zozote ambazo zinaweza kuwaweka pamoja na wakwe wao kwa njia ya ana kwa ana.

### Mafumbo ya Chemshabongo

Chemshabongo hutumiwa katika wosia kwa wavulana baada ya tohara ili kuwatayarisha kwa maisha ya utu uzima. Chemshabongo huwa na matumizi mengi ya hesabati inayochanganya akili. Katika lugha ya Kiswahili, Matei (2011) anadai kuwa chemshabongo hutumia miraba inayostahili kujazwa au hesabu inayoweza kumkanganya mtu. Haya ni mafumbo ambayo hutumia hesabati ili kumchanganya mtu na kumfanya awe makini zaidi. Kwa mfano,

Fumbo: *Nawenya chisala chitaru khukhwama khulusala lulala orema lusala khenga?*

Jibu: Chibili

Tafsiri

*Ukitaka vipande vitatu vya vijiti kutoka katika kijiti kimoja utakata kijiti hicho mara ngapi?*

Jibu: mbili.

Hili ni fumbo linalotumia hesabati kugawa kitu katika vijisehemu. Fumbo hili hutumiwa katika maisha halisi ya jamii ya Wabukusu ambapo wavulana hufunzwa jinsi ya kugawanya raslimali au kitu chochote katika jamii.

Fumbo: *Omumesi kaba khakenda khungila. Kachichanga chifuti chibili ebweni na lundi acha chitaru enyuma. Akhola ariena nio kole engo?*

Jibu: *Kayukha kanja khucha sinyumanyuma.*

Tafsiri

Fumbo: *Mlevi alikuwa akitembea njiani na alikuwa akienda futi mbili mbele na tena anaenda futi tatu nyuma. Alifanya nini ndipo afike nyumbani?*

Jibu: *Alipinduka na kuanza kuenda kinyumanyuma.*

Hili ni fumbo linalotumiwa kuwawosia wavulana katika jamii ya Wabukusu kuhusu mbinu mbalimbali za kukabiliana na changamoto katika maisha. Fumbo hili huwahimiza wavulana kuwa tatizo laweza kutatuliwa kwa kutumia kinyume cha tendo husika.

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### Hitimisho

Uainishaji ulifanywa kwa kuzingatia sifa za mafumbo zinazotofautisha aina moja ya mafumbo na nyingine. Mafumbo haya ni kama mafumbo ya maonyo, mafumbo ya majina, mafumbo ya vitendawili na mafumbo ya jazanda.

#### Mapendekezo ya Tafiti Zingine

Makala hii inapendekeza kuwa vyombo vya habari viwe vikipeperusha hotuba za wosia unaotumia mafumbo kwa wananchi ili kuwafikia watu wengi. Kwa kufanya hivi, wavulana wengi watapata ujumbe uliomo kwenye mafumbo haya na wataimarika kitabia.

#### Mapendekezo ya Utafiti Nyingine

Utafiti huu uliainisha mafumbo kwa kutumia sifa za mafumbo hayo. Kwa hivyo inapendekezwa utafiti mwingine ufanywe kuhusu vigezo vingine vinavyotumiwa kuainisha mafumbo.

### MAREJELEO

Ayiera, E. (2017). *Ufumbaji Katika Riwaya za Katama Mkangi*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Beck, R. M. (2013). Texts on Textiles: Proverbiality as a Characteristic of Equivocal Communication at the East African Coast (Swahili), *Journal of African Studies*, Vol. 17 No. 2: 131-160.

- Chemutai, J. (2016) *Mtindo Katika Hadithi Fupi ya Kisasa ya Kiswahili*, Tasnifu Ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Gathenya, E. (2018). *Mielekeo na Mtindo wa Shafi Adam Shafi Katika Riwaya za Kuli na Haini*, Tasnifu ya Uzamili Katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kipacha, A. (2014). *Misemo katika Lugha ya Magari*, Swahili Forum.
- Leech, G. H., na Short, M. H. (1965). *Style in Fiction. A Linguistic Introduction to English Fiction Prose*. England: Longman Group Limited.
- Matei, A. (2011). *Fani za Fasihi Simulizi*, Nairobi, Oxford University Press.
- Mberwa, A. (2015). *Athari ya Matumizi ya Mafumbo na Tamathali za Semi Katika Nyimbo za Ngoma ya Puuu Kwa Wazanzibari*, Tasnifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma
- Ngonyani, D. (2005). *Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii*. Swahili Forum.
- Nguta, M. (2013). *Ulinganisha wa Matumizi ya Tafida za Muktadha wa Nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Sauda, S. (1994). *Yanayouthikuyaona Mafumbo na Vijembe Vya Kiswahili*, Paper presented at the 5th Swahili-Kolloquium in Bayreuth, May 1993.
- Simiyu, F. (2015). *Mwingilianotanzu Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa*; Tasnifu ya Uzamilifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- TUKI, (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi, Oxford University Press.
- Wasike, D. (2017). *Lugha kama Rasilimali ya Jamii: Uchunguzi wa Redio za Fm Zinazotumia Kibukusu katika Kaunti wa Bungoma*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Moi.